



MKATABA WA UJENZI WA PICNIC SITE PANDE

KATI YA PORI LA AKIBA PANDE

NA

NDUGU ANTHONY ARNOLD KOMU

DISEMBA, 2021

MKATABA WA UJENZI WA PICNIC SITE- KITUO CHA PANDE

Mkataba huu umeingiwa leo tarehe 30..... Mwezi 12....mwaka 2021, BAINA ya **Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – Pori la akiba Pande** yenyе ofisi yake eneo la Morogoro **S.L.P 2856 Morogoro** (hapa ataitwa ‘TAWA’-Pande) kwa upande mmoja.

NA

Ndugu **ANTHONY ARNOLD KOMU S.L.P 404, Dar es Salaam - SIMU 0713615603** wa **Dar es Salaam** ambaye kwa mkataba huu (ataitwa ‘mjenzi’) kwa upande wa pili.

1. UTANGULIZI

TAWA ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea Iliyoanzishwa chini ya Sheria ya kuhifadhi Wanyamapori No.5 ya Mwaka 2009, kusimamia wanyamapori wanaopatikana nje ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro ambayo inatekeleza miradi yake mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa picnic site katika Pori la Akiba Pande.

Mjenzi ni mwenye utaaliam wa kujenga Majengo na ukarabati wa miundo mbinu mbalimbali ambaye anamiliki kikundi cha ufundi chenye ujuzi na uzoefu wa kazi husika.

TAWA iko tayari kumpatia Mjenzi kazi za utendaji pekee (labour only) ili afanye kazi yote ya kujenga hadi kukamilisha kazi zote tajwa katika mkataba huu kama itakavyoinishwa.

Mjenzi ameona kazi husika na kuelewa ukubwa na mahitaji ya kazi ikiwa ni pamoja na ubora unaotakiwa (Specification).

Na. Mfululizo	Maelezo ya Kazi
	MSINGI
A	Kusafisha eneo
B	Kuchimba msingi
C	Kuondoa takataka zilizochimbwa eneo la kazi
D	Kurudishia udongo kwenye msingi
E	Kurudishia kifusi kwenye eneo la ndani ya msingi
F	Kupanga mawe kwenye jingo
G	Kupulizia dawa kwenye eneo la ndani la msingi kwa ajili ya mchwa
H	Kupulizia dawa pembezoni mwa msingi kwa ajili ya mchwa

J	Kumwaga zege au mchanga kwenye msingi
K	Kumwaga zege jamvi
L	Kumwaga zege kwenye msingi
M	Kufunga nondo
N	Kutengeneza box kwa ajili ya zege
P	Kujenga kuta za msingi
Q	Kuweka nailoni juu ya mawe
R	Kupiga plaster kwenye msingi
S	Kupaka rangikwenye msingi
	BOMA
A	Kumwaga zege la bimu/Linta
B	Kufunga nondo za bimu ya juu/linta
C	Box za bimu/linta
D	Ujenzi wa kuta za boma na zinginezo kama kwenye mchoro
E	Ujenzi wa vimbweta kwa maelekezo ya mhandisi na michoro
	MILANGO
A	Doors saizi 800*2100mm high;D2
	Kupachika Fremu
B	45*100mm fremu
	Kupachika Vitas
D	Kufunga mlango na vifaa vyake
E	Vizuizi
	MADIRISHA
	Kupachika madirisha ya Aluminium
A	Saizi 700*700mm high
	KAZI ZA CHUMA
	Mild steel;protected from rust by applying three coats of zinc chromate primer and full coats of gloss paint:
B	Kupachika grills kwenye madirisha
C	Kutengeneza mabomba ya chuma kwenye vimbweta na kupachika kwa maelekezo kutoka kwa mhandisi
D	Kutengeneza henga za chuma za vimbweta na kupachika kwa maelekezo kutoka kwa mhandisi
	PAA
	KUPIGA BATI LA IT ALAF
A	Kuweka/kupiga paa(bati)
B	Kufunga nondo na box kwenye paa kwa ajili ya zege
C	Kumwaga zege la paa
D	Kutengeneza paa za vimbweta kwa maelekezo ya mhandisi

	KENCHI
E	Kupiga/Kufunga kenchii
FINISHING	
PLASTA NDANI NA NJE	
A	Kupiga plasta kuta za ndani pamoja na nje
B	Kupiga plasta kuta za nje
C	Kupiga plasta kwenye vimbweta
FINISHING YA DARI	
D	Kupiga brandaring
E	Kupiga gypsum bodi
F	Kupiga mikanda ya gypsum bodi
FINISHING YA SAKAFU	
	Kuweka sakafu levelling
G	Kuweka timanzi kwenye sakafu na kufanya levelling
H	Kuweka timazi kwenye kuta na kufanya levelling
KAZI ZA TILES	
J	Kuweka tiles kwenye sakafu
K	Kuweka tiles kwenye kuta za chooni
KUPIGA RANGI	
A	Kupiga rangi kuta za ndani pamoja na dari
B	Kupiga rangi kuta za nje
C	Kupiga rangi kwenye grili za madirisha na vimbweta
D	Kupiga rangi kwenye milango na frame
MFUMO WA MAJI SAFI NA TAKA	
A	Kupachika masinki ya wanaume(Urinal bowls)
B	Kupachika vyoo vya kuchuchumaa
C	Kupachika choo cha walemauvu
D	Kupachika mabeseni ya kunawia mikono
E	Kupachika toilet paper holders
F	Kupachika vifaa vya kunawia(stuff) Pamoja na mabomba
G	Kupachika floor drainage
H	Kupachika vioo
J	Kujenga mashimo ya taka mawili septic na soakaway pit kwa maelekezo ya mhandisi
K	Kujenga chemba za vyoo kutokana na maelezo ya mhandisi
L	Kufunga mabomba yote Pamoja na vifaa vyake kwenye miundombinu yote ya maji safi na taka
UMEME	
A	Kutindua kuta kwa ajili ya umeme
B	Kuweka bomba na metal boxes

C	Kuweka bomba kwenye dari na vifaa vingine vidogo
D	Kufanya wiring jengo zima
E	Kuweka vifaa vya mwisho kwenye umeme(i.e switches, taa, feni n.k)

3. SASA INAKUBALIKA KWA PANDE ZOTE KAMA IFUATAVYO:

A. MALIPO

TAWA itamlipa mjenzi jumla ya **TZS. 11,000,000.00** /= (**Shilingi za kitanzania Milioni Kumi na Moja tu**) zitakazolipwa kwa awamu Tatu.

1. Malipo ya awali asilimia 30% (**Shs. 3,300,000/=**) **Milioni Tatu Tatu tu** zitakazolipwa ndani ya siku ishirini na nane (28) baada ya kusaini mkataba huu na kuanza kazi.
2. Malipo ya pili asilimia 30 % (**Shs. 3,300,000/=**) **Milioni Tatu tu** yatalipwa baada ya kazi za kuta, sakafu, zege na paa
3. Malipo ya tatu na ya mwisho asilimia 40 % (**Shs. 4,400,000/=**) **Milioni Nne tu** yatalipwa baada ya kazi kukamilika

B. MUDA

Muda wa kutekeleza mradi huu ni siku tisini (90) ikijumlisha pia siku za mwisho wa juma. Muda wa kumaliza kazi unaibana TAWA na Mjenzi na hivyo mjenzi anatakiwa kufanya kazi tajwa bila kusimama. Mjenzi atasimamisha kazi endapo vifaa vya ujenzi (building materials) vitakuwa vimeisha au hali ya hewa kutoruhusu kufanyika kwa kazi.

C. VIFAA VYA UJENZI (BUILDING MATERIALS)

TAWA itawajibika kuleta vifaa vya ujenzi (building materials) vinavyohitajika kwa wakati kwa ajili ya ujenzi wa *picnic site*. Vifaa vyote vitafikishwa eneo la ujenzi Kutokuwepo kwa vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kazi itakuwa sababu mojawapo ya mjenzi kusimamisha kazi.

D. USIMAMIZI WA UJENZI.

Kutakuwa na msimamizi wa mjenzi. Kwa kuwa kazi hii ni ya TAWA msimamizi wa ubora wa kazi atatoka TAWA. Msimamizi atakuwa akitoa maelekezo juu ya utendaji kazi ili kupata ubora unaohitajika na kwamba atakuwa akishauriana na Mjenzi juu ya ubora wa ujenzi. Msimamizi pia atakuwa na jukumu la kutunza muda wa mradi.

Utunzaji wa muda utahusu kujadiliana na mjenzi juu ya hatua stahiki za kufanya ili kazi isichelewe kutokana na mpango kazi wa mradi.

E. MITAMBO.

Pale itakapohitajika, Tawa itatoa vifaa ili kukamilisha mradi kwa wakati. Mjenzi atawajibika kutoa mahitaji hayo mapema ili maandalizi yafanike kwa wakati

F. USALAMA KAZINI.

Mjenzi atawajibika kwa masuala yote ya usalama kazini. Hii itajumuisha usafi wa eneo la mradi ikiwa ni pamoja kuhifadhi na kutunza mazingira ya eneo husika.

G. KUTUNZA VIFAA

Vifaa vyote kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huu vitatunzwa na mtunza stoo wa TAWA. Mtunza stoo atakuwa na jukumu la kuhakikisha usalama wa vifaa vyote vinavyotumika kwenye ujenzi.

H. KUCHELEWA KWA MALIPO NA VIFAA.

Kwa kuwa mjenzi anajitegemea kwa kila kitu suala la gharama za kujikimu linategemea sana muda. Hivyo upatikanaji wa fedha za malipo kwa watenda kazi ni muhimu. Endapo kazi itasimama kwa sababu zilizosababishwa na TAWA, Mjenzi atachukua moja ya hatua zifuatazo:

- (a) Atamuarifu msimamizi juu ya hali hiyo.
- (b) Atasimamisha kazi kwa muda.

I. KUCHELEWESHA KAZI.

Endapo kutatokea ucheleweshaji wa kazi kwa sababu ambazo hazitokani na ucheleweshaji wa TAWA, Mjenzi atawajibika kukatwa malipo yake kiasi cha shilingi 10,000 kwa kila siku mpaka kazi itakapokamilika.

J. MGOGORO.

Endapo kutatokea mgogoro wakati wa utekelezaji wa kazi hii, pande zote mbili za mkataba zitakubaliana kwamba zitatafuta usuluhishi kutoka ndani ya jumuia ya watu wa ujenzi na au taasisi za ujenzi ili kumaliza tatizo husika.

K. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa iwapo upande wowote utaonekana kutotimiza makubaliano yaliyofikiwa ikiwa ni pamoja kufanya kazi kwa kiwango cha chini kuliko ilivyotarajiwa. Ikiwa Mkataba utasitishwa pande husika italazimika kulipa tozo ilioainishwa kwenye Ibara I hadi tarehe ya kusitishwa kwa Mkataba huu.

L. SHERIA ZITAKAZOTUMIKA PAMOJA NA MAHAKAMA ZENYE MAMLAKA

Mkataba huu utasimamiwa na Sheria za Tanzania na Mahakama za Tanzania zitakuwa na Mamlaka ya kusikiliza Shauri litakalotokana na Mkataba huu.

Kwa kuthibitisha makubaliano haya tunaweka sahihi zetu hapa.

TAWA –PANDE

SAHIHI.....*H. Buretti*

JINA.....*HONEST J. BURETTA*

CHEO.....*MKUU WA KITMO*

KWA MJENZI

SAHIHI.....*[Signature]*

JINA.....*ANTHONY ARNOLD*

CHEO.....*MJENZI MKUU*

SHAHIDI WA MAMLAKA

SAHIHI.....*M. Ali*

JINA.....*Mohamed A. Madarwa*

CHEO.....*Concertator II*

SHAHIDI WA MJENZI

SAHIHI.....*P. Chege*

JINA.....*NOEL SANGAWE*

CHEO.....*MGT/1/21*

MWISHO.

ANTHONY TRAOWD,
S.L.P 404,
DAR-E.S-STAFF,
30/12/ 2021

KAMISHTA WT KILIFADI,
MANAKA YT KAMALIZI WT WATYAMAPORI TUSIKI,
S.L.P 2658,
MOROGORO.

YAH! KUKUBTHI UJFUZI WT PICNIC SITE
Beja kiciwa cha harsani hapo juu nini
tutwony kmosi nine kubali kijenga picnic Site
inayo gadibana pori la akiba Poude kwa glarama
ya shillingi millioni kumi na moja (11,000,000Tsh).

Nitafanya kati kwa nadilifu na ustasi mtakwa.
Wato batika wenzie wa Taifa.

ANTHONY TRAOWD.

